

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

05

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Time: 2:30 Hours.

MAJIBU

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali matano (5)
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama thelathini (30) na sehemu B ina alama ishirini (20).

maktaba.tetea.org



SEHEMU A (Alama 30)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku ulichopewa.

(i) Ni kifaa gani hutumika kuhifadhia vyakula kuepuka visiharibike?

- A. Kabati
- B. Jokofu
- C. Chupa
- D. Hotipoti

B. Jokofu

Jokofu hutunza vyakula kwa baridi hivyo kuzuia kuoza na kuharibika kwa haraka.

(ii) Seti ipi haiwakilishi aina ya majiko?

- A. Jiko la mkaa, jiko la umeme na jiko la mafuta ya taa
- B. Jiko la umeme, jiko la mafuta ya taa na jiko la gesi
- C. Jiko la mkaa, jiko la umeme na jiko la gesi
- D. Jiko la umeme, mkaa na moto

D. Jiko la umeme, mkaa na moto

Mkaa na moto si aina za majiko bali ni vyanzo vya nishati.

(iii) Ni kifaa kipi hutumika kupima uzito sahihi wa sukari?

- A. Kikombe
- B. Sahani
- C. Mzani
- D. Silinda kipimo

C. Mzani

Mzani hutumika kupima uzito sahihi wa vitu mbalimbali.

(iv) Ni sifa ipi ya viumbe hai hutofautisha mimea na wanyama?

- A. Kutoa uchafu
- B. Kufa
- C. Kujongea
- D. Kukua

C. Kujongea

Wanyama hujionyesha kwa uwezo wa kujongea kutoka sehemu moja kwenda nyingine, tofauti na mimea.

(v) Nini kazi ya mashine?

- A. Kurahisisha kazi
- B. Kufanyia mawasiliano
- C. Kuzalishia bidhaa
- D. Kunyanyua mizigo

A. Kurahisisha kazi

Mashine hutengenezwa ili kufanya kazi iwe nyepesi na ya haraka.

2. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuoanisha maelezo kuhusu dhana mbalimbali za nishati ya joto katika Orodha A na dhana husika katika Orodha B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Orodha A	Jibu	Orodha B
(i) Namna joto linavyosafiri katika chuma	(E)	E. Mpitisho
(ii) Kusambaa kwa joto katika maji	(F)	F. Msafara
(iii) Namna joto la jua linavyofika duniani	(D)	D. Mnururisho

(iv) Maada inavyosafirisha joto kwa haraka	(A)	A. Yabisi
(v) Chanzo cha asili cha joto	(B)	B. Jua

3. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku lifuatalo na kuliandika katika nafasi uliyopewa.

Maneno: Oksijeni, Chakula, Maji, Hewa, Ardhi, Kabonidayoksaidi, Mimea

(i) Ni gesi ipi hutumiwa na mimea kama malighafi?

Kabonidayoksaidi

(ii) Kipi ni matokeo ya muunganiko wa gesi mbalimbali?

Hewa

(iii) Nini chanzo cha chakula kwa viumbe hai?

Mimea

(iv) Ni aina ipi ya gesi inahitajiwa moja kwa moja na viumbe hai?

Oksijeni

(v) Nini chanzo cha virutubisho kwa ajili ya kazi mbalimbali za mwili?

Chakula

SEHEMU B (Alama 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

4. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

Tunaweza kuyaona maji tunayotumia ni salama kwa macho, lakini yasiwe salama kwa afya zetu. Hii ni kwa sababu maji yanapotiririka ardhini huchukua udongo na wakati mwingine huchukua vijidudu vya magonjwa. Kwa hiyo, tunashauriwa kuchemsha maji ili kuua vimelea vya magonjwa. Baada ya kuchemsha, inatupasa kuyachuja kwa kutumia kitambaa safi ili kuondoa uchafu. Aidha, maji yaliyochemshwa na kuchujwa

huhifadhiwa katika chombo safi na chenye mfuniko ili yasichafuke. Haya sasa ni maji safi na salama.

(i) Kwanini ni muhimu kuchemsha maji?

Ni muhimu kuchemsha maji **ili kuua vimelea vya magonjwa.**

(ii) Ni kwa namna gani maji hupata vijidudu?

Maji hupata vijidudu **yanapotiririka ardhini na kuchukua udongo na vijidudu.**

(iii) Nini kifanyike ili kufanya maji yawe safi na salama?

Ni lazima **kuchemsha na kuyachuja maji kwa kitambaa safi.**

(iv) Kifaa gani hutumika kuchuja maji?

Kitambaa safi hutumika kuchuja maji.

(v) Ni kwanini maji huhifadhiwa katika chombo chenye mfuniko?

Huhifadhiwa hivyo **ili yasichafuke tena.**

5. Chunguza picha zifuatazo kisha jibu vipengele (a) hadi (e).

(a) Nini majina ya vifaa vinavyoonekana katika picha?

(i) **Wembe**

(ii) **Mswaki**

(b) Ni ugonjwa gani huambukizwa kwa sababu ya kushirikiana katika kutumia vifaa hivyo?

Ugonjwa unaoweza kuambukizwa ni **UKIMWI.**

(c) Ni njia gani hutumika kumbaini mtu aliyeathirika na ugonjwa ulioutaja katika kipengele (b)?

Njia ni **kupima damu hospitalini.**

(d) Ni njia ipi nyingine maambukizi ya ugonjwa ulioutaja katika kipengele (b) hutokea? Maambukizi hutokea pia **kupitia kujamiiana bila kinga.**

(e) Kwanini inashauriwa tusimtene mtu anayeugua ugonjwa ulioutaja katika kipengele (b)?

Ni kwa sababu **ugonjwa huo hauambukizwi kwa kushirikiana chakula au kuishi pamoja, na mgonjwa anahitaji msaada na faraja.**